**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI

**SHULE YA SEKONDARI**
**EMANUEL NCHIMBI**
**S.L.P 633**
**SONGEA**

**JULAI 2026**
**SONGEA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**Namba za simu:**

**Mkuu wa Shule: 0755 675 356**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0621 919 319**

**Patron: 0762 084 165**

**Shule ya Sekondari Emanuel Nchimbi**

**S.L.P 633**

**Songea.**

**Tarehe …. / …. / 2026.**

**Mzazi / Mlezi wa Mwanafunzi ………………………………**

**……………………………………………………………….**

**S.L.P ……………**

**……………………………**

**Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WAVULANA EMANUEL NCHIMBI - SONGEA KWA KIDATO CHA TANO MWAKA 2026/27.**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2026/27 na atasoma tahasusi ya …………….

Shule ya Sekondari Emanuel Nchimbi ipo umbali wa Kilometa 7 Magharibi mwa Mji wa Songea. Usafiri wa basi kutoka kituo kikuu cha mabasi cha **Shule ya Tanga** unapatikana kwa nauli ya Shilingi 900/= (Dala dala) kuelekea mjini. Shuka kituo kiitwacho **MAUKI.** Hapo pana usafiri wa daladala kwa shilingi 900/= au pikipiki kwa shilingi 3,000/= kufika shule. Hakikisha umechukua fomu ya Maelekezo ya kujiunga na shule (Joining Instructions), itakayokutambulisha kama mwanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wavulana Emanuel Nchimbi kwa Kondakta / Dereva wa mabasi utakayotumia kusafiri kufika Songea, watakusaidia namna ya kufika shuleni salama. (Tafadhali zingatia maelekezo haya)

Muhula wa masomo utaanza tarehe ………. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe …….. Mwisho wa kuripoti ni tarehe ……….. Unatakiwa kufika shuleni tarehe husika. Mwanafunzi atakayechelewa kuripoti pasi na taarifa ya kuchelewa kwake atakuwa amepoteza nafasi hii.

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule ni suruali mbili(2) nyeusi zisizo bana zenye marinda mawili mbele na mfuko mmoja nyuma (upana chini ya miguu uwe inchi 16 na iwe na turnup ). Shati mbili (2) nyeupe mikono mirefu (tetroni – tomato) na Tai (2) lightblue nyembamba. **(Tai zinaweza kupatikana shuleni kwa gharama ya Tsh.5,000/= kwa anayehitaji)**

ii. Sare ya michezo
- Mwanafunzi aje na Tracksuit nyeusi yenye fito tatu nyeupe kwa anayependa zinapatikana karibu na shule **kwa gharama ya Tshs 27,000/= .**
- Viatu vya michezo jozi moja (1)**.**
- Mwanafunzi aje na T-shirt ya jezi ya blue isiyo na maandishi. Kwa atakayependa zinapatikana karibu na shule kwa gharama ya Tsh. 15,000/=

iii. Viatu vya shule ni vya ngozi vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi na sio mchongoko.

iv. Soksi jozi mbili au zaidi nyeusi.

v. Sweta rangi ya dark bluu moja au zaidi zenye V shape shingoni .

vi. Mikanda 2 myeusi ya ngozi ya kuvalia suruali.

**TANBIHI:**

**Mzazi / Mlezi na mwanafunzi tafadhali zingatia vipimo na maelekezo yalivyoainishwa. Mwanafunzi atayeshona / kununua / kuja na sare za shule kinyume na vipimo, rangi na aina ya kitambaa tulichokielekeza mzazi atalazimika kumshonea / kumnunulia nyingine kulingana na maelekezo ya shule.**

**Mzazi unashuriwa ili kuepuka utofauti wa rangi, aina ya kitambaa na vipimo, unashauriwa kuja kushona / kununua huku wakati anaripoti**

**Nguo za nyumbani haziruhusiwi kabisa, anaporipoti awe amevaa sare ya shule (Tracksuit).**

**<u>MAHITAJI YA BWENI.</u>**

**i.** Mashuka jozi mbili (2) light blue – kwa ajili ya kutandika kitandani.

**ii.** Blanketi la kawaida (student size 1), Mto, foronya, taulo na chandarua rangi ya bluu na taulo moja(1) au mbili (2).

**iii.** Godoro moja la futi 2.5 kwa 6 lenye cover.

**iv.** Shuka za kulalia mbili za futi $2^{1/2}$ x 6 (rangi yoyote).

**v.** Sandle / Sendo za kiume za kawaida (Zisiwe na soli kubwa midundiko) za kushindia.

**iv.** Tochi moja kwa ajili ya dharura, mwanga unapokosekana. (yenye kutumia seli kavu au solar **(isiwe ya kuchaji na umeme.)**

**v.** Nguo za kushindia:
- Suruali 2 rangi ya ugoro (suruali upana miguuni uwe inchi 16 na turnup).
- Aje na 15,000/= kwa ajili ya T-shirt yenye nembo ya shule**.**

**vi.** Vyombo vya chakula container lenye mfuniko / Sahani, Bakuli, Kikombe na Kijiko (Vinapatikana kwenye duka la shule).

**vii.** Awe na sanduku (chuma au la bati) linalofunga vizuri kwa ajili ya kutunzia vitu vyake likiwa na kufuli imara.

viii. Nguo za ndani (ziwe boksa sio bukta / kaptula) na vesti nyeupe za kutosha.
ix. Kandambili / Ndala kwa ajili ya kuogea.
x. Aje na Sabuni, Mafuta ya kupaka ya kawaida / mgando **(Mafuta yenye Cream au marashi yenye harufu kali hayaruhusiwi).**

**NB: Mahitaji / Vifaa hivi vyote vinaweza kupatikana shuleni kwa anayehitaji.**

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:**

i. Madaftari ya kutosha kwa masomo husika (kaunter books quire 3au 4 kuanzia kumi.
ii. **REAM (A4)** mbili (2) kwa mwaka.
iii. Vitabu vya masomo kwa tahasusi husika. Vimeainishwa mwishoni mwa fomu hii.
iv. Scientific calculator na graph pad moja kwa mwanafunzi watakaosoma Geography.
v. Aje na OXFORD ADVANCED LEANERS DICTIONARY-Kwa somo la Kiingereza na KAMUSI YA KISWAHILI SANIFU,OXFORD-Kwa somo la Kiswahili. **Ni lazima kwa wanafunzi wa Masomo ya Lugha.**
vi. Ndoo 2 (kubwa 1 na ndogo 1) zenye mifuniko.
vi. Vifaa vya usafi kwa wote:- Fagio ya chelewa mbili (2) kwa muhula, nne (4) kwa mwaka.
- **HGK -** Jembe 1, Kwanja 1, Softbroom 1, Drier 1na Reki 1
- **HKL -** Jembe 1, Kwanja, Hardbroom 1,Drier 1na Mopa

**(Vifaa vyote anaweza kuvipata kwenye duka la shule)**

vii. Hakikisha mtoto wako ana Bima ya Afya, kwa asiyekuwa nayo alete Tsh.50,400/= kwa ajili ya Bima ya afya kwa mwaka ni **Lazima**. Fedha hii sio sehemu ya mchango wa shule, hivyo alete fedha taslimu (Asiingize kwenye akaunti ya shule).

**2.3 Michango mbalimbali.**

| **Na** | **Aina ya Michango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | **65,000/=** |
| 2 | Tahadhari | **5,000/=** |
| 3 | Nembo | **5,000/=** |
| 4 | Kitambulisho cha Shule | **5,000/=** |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Michango yote kwenye 2.3 iwekwe kwenye akaunti namba **61810017203 NMB.** Jina la akaunti ni **Shule ya sekondari EMANUEL NCHIMBI / EMANUEL NCHIMBI SECONDARY SCHOOL.** Mwanafunzi aje na **<u>Nakala halisi ya hati za malipo (Original Bank Pay in Slip zilizoandikwa jina la mwanafunzi sio vinginevyo).</u>**

**FEDHA ZA MATUMIZI YA MWANAFUNZI.**

Mzazi anashauriwa kumpatia mwanafunzi fedha za kutosha kwa matumizi yake binafsi. Aidha mwanafunzi haruhusiwi kuweka fedha bwenini, akabidhi ofisi ya Mhasibu atunziwe. Vilevile Mzazi/Mlezi kama atataka kutuma fedha ya matumizi ya mwanafunzi atume kupitia kwa namba zifuatazo.

Mkuu wa Shule: **0755 675 356**, Makamu Mkuu wa Shule: **0621 919 319,** Mhasibu wa Shule: **0769 696 069,** Ofisi ya Malezi: **0762 084 165**-Mwl.Pores P.Kayombo na **0716 171 704**-Mwl.Salehe A.Bakari

**JAMBO LA MUHIMU: Mzazi ukituma pesa kwa mwanafunzi kupitia kwa mwalimu yeyote andika ujumbe mfupi (sms) wa kumtambulisha mhusika,** ***Mfano; Nimetuma sh……………../= ya mwanafunzi <u>Adam Hassan Beatus</u> kidato cha tano. Ni vyema na ni vizuri ukawasiliana na unayemtumia pesa, kabla ya kutuma. Hii ni kwa Fedha za Matumizi tu.***

**3. Sheria na Kanuni za Shule**.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais—TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku ( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**Aidha mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

**NB: NI MARUFUKU KWA MWANAFUNZI KUMILIKI, KUTUMIA AU KUKUTWA NA SIMU YA MKONONI KATIKA MAZINGIRA YA SHULE. IKIBAINIKA, MBALI NA ADHABU NYINGINE, MWANAFUNZI ATATAKIWA KULIPA GHARAMA YA UHARIBIFU. (Atakayopangiwa Kulingana na madhara yaliyojitokeza au yanayoweza kujitokeza).**

a. Kwa Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa.

b. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;
c. Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Kwa ruhusa ya Msiba au Ugonjwa).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na**:

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa,
xvi.Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi,

**MUHIMU: Mwanafunzi atakayebainika kuruka / kuchora / kukwangua na kuandika ukutani katika majengo ya shule atatakiwa kulipa Ndoo moja ya Rangi (Silk) lita 20 pamoja na gharama nyingine kulingana na uharibifu.**

**MZAZI ZINGATIA:**

a. Mawasiliano yoyote kati ya mwanafunzi na mzazi/mlezi yafanyike kupitia Ofisi ya Mkuu wa Shule, Makamu Mkuu wa Shule na Ofisi ya Malezi tu. Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na simu ya mkononi.
b. Shule haina utaratibu wa kuwaona wanafunzi isipokuwa mzazi ataitwa na uongozi wa shule kama kuna ulazima wa kufanya hivyo. Au kila mwisho wa mwezi kwa kibali maalumu.
c. Mzazi/Mlezi kutompa mtoto fedha nyingi ambazo zitamfanya apoteze utulivu wa maisha ya shule na kuvunja sheria za shule.
d. Shule ina utaratibu wa kushughulikia usafiri kwa wanafunzi kipindi shule inapofunga. Hivyo mzazi / mlezi utapewa taarifa kabla ya shule kufunga, mapema iwezekanavyo ili kuandaa nauli ya mtoto.
e. Mzazi hakikisha unapima afya ya mwanao kwa uaminifu ili kuepuka usumbufu wakati wa masomo.
f. Iwapo mwanao ana ugonjwa unaomsumbua mara kwa mara, tafadhali aje na vyeti pamoja na dawa anazotumia na kukabidhi ofisi ya malezi. Hii itarahisisha shule kumhudumia. Usipofanya hivyo shule itashindwa kumhudumia. Usifiche ugonjwa utapokelewa tu, kupata elimu ni haki yako.
g. Mwanafunzi anaruhusiwa kuleta pasi ya mkaa kwa ajili ya kunyoshea ngua zake. Ni marufuku mwanafunzi kuwa na kutumia pasi ya umeme ama kifaa chochote kinachotumia umeme. Ikibainika hatua kali zitachukuliwa dhidi yake ikiwemo kusimamishwa shule.

h. Shule itakapokuwa imefunga, likizo zote mwanafunzi atatokea shuleni moja kwa moja kwenda kwa mzazi wake (nyumbani kwao) na shule itakapofungua atatokea nyumbani kwao ( kwa wazazi) moja kwa moja kuja shuleni.
i. Mwanafunzi haruhusiwi kuja na kumiliki simu au kifaa chochote kinachohusiana na simu hata kama anatoka mbali. (AKIJA NAVYO ATARUDISHWA NYUMBANI KURUDISHA KIFAA HICHO)

**TAALUMA**

**(a)** Mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi vyote vya masomo na kufanya mazoezi yote anayopewa na mwalimu wa somo husika. Asipofanya hivyo atapewa adhabu ikiwemo kurudishwa nyumbani.
**(b)** Mwanafunzi anatakiwa apate alama zisizopungua 60 kwa kila somo analosoma,akishindwa kufikia wastani huo ataadhibiwa.
**(c)** Mwanafunzi anatakiwa aje na cheti cha matokeo ya ufaulu ya kidato cha nne.
**(d)** Mwanafunzi aje na cheti cha kuzaliwa.
**(e)** Mzazi unatakiwa kumnunulia mwanao vitabu kulingana na tahasusi yake kwa kadri utakavyoweza. (Orodha ya vitabu imeambatanishwa kurasa za mbele).

**CHAKULA:**

Shule hutoa chakula ambacho huliwa na Watanzania wote, ambacho Serikali inapendekeza kuliwa na mwanafunzi. Pia shule haitoi kibali kwa mwanafunzi kujipikia hivyo asilete chakula kama mchele,unga,biskuti, mkate, Sukari, kinywaji cha aina yoyote n.k na haturuhusu mwanafunzi kununua aina yoyote ya chakula / kinywaji nje ya shule.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu.**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi / Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makossa ya jinai.
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sharia, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4 passport size) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

**Tafadhari soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.**

**Saini ya Mkuu wa Shule:**..........

**Jina la Mkuu wa Shule: ALETAS N.MSUHA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule:** MKUU WA SHULE EMANUEL NCHIMBI SEKONDARI S.L.P 633 SONGEA-RUVUMA

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama**

**walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.**

**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI / MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:**

- **Mkuu wa shule-----------------------0755675356**
- **Makamu Mkuu wa Shule-------- 0621919319**
- **Mwandamizi Taaluma ------------0620360595**
- **Mwandamizi Malezi ---------------0621529727**

**FORM A**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRIME MINISTERS' OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

**The headmaster,**
**Emanuel Nchimbi Secondary School,**
**P.O. Box 633,**
**SONGEA.**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**To Medical Officer**
**……………………………….**
**……………………………….**

Please examine,
Mr. …………………………………………………………as to his physical and mental fitness for admission as a form FIVE student for the Academic year 2025/26.

Your sincerely,

**THE HEADMASTER**

THE HEADMASTER
EMANUEL NCHIMBI SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 633
SONGEA-RUVUMA

The Headmaster, I have examined
Mr. …………………………………………………………as shown below and consider that he is physically and mentally **fit** / **unfit** for admission to pursue a fulltime secondary education. (To be completed by a medical Officer).

1. Vision with/without glasses: Right………………………… Left …………………………..
2. Blood pressure………………………… Hemoglobin………………
3. Hearing ………………………
4. (a)Urinalysis:………………… (b) Sugar …………………..

5.(a)Venereal Diseases test:…………….. (b) Bilharzias…………………………..
6. Neurosis:…………………………………
7. Is there any abnormality of:
(a) The heart ……………………(b) Lungs …………………. (c) The spleen ……………
8. Are there any serious disease e.g leprosy, Asthma, Diabetes, etc. …………………..
ADDITIONALL INFORMATION (If any) e.g. Physical defects, impairment(s) e.g. arm, leg etc. infection chronic or family disease etc. ……………………………………………………..

I certify that the above is fit to pursue further education as stated above.

Signature:…………………… ……………… Designation:………………

Station:………………………..Date:……………….. Official Stamp: …………………

**KIAMBATANISHO B**

## FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI PAMOJA NA AHADI YA UTII WA SHERIA ZA SHULE.

### KUMBUKUMBU MUHIMU ZA MWANAFUNZI.

1. Jina kamili la mwanafunzi ……………………………….………………
2. Anuani ya nyumbani S. L. P………………… Wilaya…………………..
3. Mahali alipozaliwa:

   Kijiji/Mtaa………………… Kata …………… Taarifa ……..…………
4. Mahali unapoishi kwa sasa:

Kijiji/Mtaa………………Kata……………………Tarafa……………

   Wilaya……………………………… Mkoa…………………………
5. Shule ya sekondari uliyotoka / kumalizia kidato cha nne ..………………
6. Dini / Dhehebu lako ………………………………… Kabila …………………………………

### AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi Mwanafunzi**…………………………………………………** nakubali kwa dhati nafasi niliyopewa na Taifa langu ya kujiunga na Shule ya Sekondari Emanuel Nchimbi na nathibitisha kuwa tarifa nilizotoa ni za kweli. Nitafuata sheria zote za shule kama zilivyotolewa na zitakazotolewa na Uongozi wa Shule. Naahidi mbele ya mzazi/mlezi wangu kuwa nitajitahidi upeo wa uwezo wangu kuwa mwanafunzi mwema, nitashirikiana na Walimu, Wafanyakazi wasio walimu pamoja na wanafunzi wenzangu katika kila jambo lenye manufaa kwa Shule na Taifa kwa ujumla

Saini ya Mwanafunzi: ……………………… Tarehe:……………………

**KIAMBATANISHO C**

SHULE YA SEKONDARI YA WAVULANA EMANUEL NCHIMBI - SONGEA

FOMU MAALUM INAYOONYESHA TAARIFA ZA NDUGU WA JIRANI / KARIBU NA MWANAFUNZI

Ndugu wa karibu na mwanafunzi: Hakikisha unaandika majina kamili matatu (3) na anwani zao.Hii inasaidia shule kutoataarifa endapo tatizo litatokea . Hatutaki majina ya ndugu wa bandia. (Bandika picha za wahusika kwenye visanduku)

**1.** (a) Jina : ________________________

(b) Uhusiano: ___________________

(c) Anwani: ___________________

**(d)** Namba ya Simu: ________________

Jina la Mwenyekiti wa Mtaa/Kijiji: ___________________________

Muhuri : __________

Namba ya simu: _____________________

**2.** (a) Jina :___________________

**(b)** Uhusiano: ___________________

**(c)** Anwani:____________________

**(d)** Namba ya Simu:_______________

Jina la Mwenyekiti wa Mtaa/Kijiji:_____________________

Muhuri: ___________________

Namba ya simu: _____________________

**3.** (a) Jina :________________________

**(e)** Uhusiano: _________________________

**(f)** Anwani: ___________________________

**(g)** Namba ya Simu: ____________________

Jina la Mwenyekiti wa Mtaa/Kijiji: ______________________________

Muhuri: _______________________

Namba ya simu: _________________________

**AHADI YA MZAZI**

Mimi Mzazi wa **……………………………………………..** naahidi kwamba nitatimiza wajibu wangu kwa mwanangu na kumsititizia kufuata taratibu zote za shule kama ilivyoelekezwa na itakavyoelekezwa na Uongozi wa shule ili kumpa mwanangu malezi bora yatakayomwezesha kuwa raia mwema na bora wa Taifa letu.

Saini ya Mzazi/Mlezi: ………………………… Tarehe: ……………………

**ORODHA YA VITABU VYA ZIADA AMBAVYO ANAWEZA KUJA NAVYO.**

**1. HISTORY**

- History For Advanced Student Book – T.I.E 2024
- Essentials In Advanced Level History paper 1&2 – Salehe Yasin
- Advanced Level History 1&2 – Idrisa Msuya

**2. GEOGRAPHY**

- Practical Geography For Advanced Secondary School, Students Book – T.I.E 2022
- Physical Geography For Advanced Secondary School, Students's Book – T.I.E 2022
- Physical Geography In Diagram – RB.Bunnet 1975.
- McDougal Little World Geography – Daniel D.Arreola et-al. 2007

**3. ENGLISH LANGUAGE**

-English Language for Advanced Level - TIE

**PLAY**

-The Government Inspector – N.Gogol

-An Enemy of the People – H.Ibsen

**NOVEL**

-An Animal Farm – G.Orwell

- The Opportunist Elite –

**POETRY**

-Poets of Africa – Lament of the Silent & Other Poems

-Summons – R.S.Mabala et al

**4. KISWAHILI**

- Kiswahili Shule za Sekondari, Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tano - TIE

**RIWAYA**

- Dunia Uwanja wa Fujo – E.Kezilahabi
- Ua la Faraja –W. E. Mkufya
- Mirathi ya Hatari – C.G.Mng'ong'o
- Wasifu wa Siti Binti Saadi – Shaban Robert

**TAMTHILIYA**

- Mkwawa wa Uhehe – M.M.Mulokozi
- Shujaa Mirambo – E.Mbogo
- Usalili Mjini – F.Imbuga

**USHAIRI**

- Fumbo Linaloelea – N.Nyangwine
- Malenga wa Ziwa Kuu – Walah Bin Walah
- Andamo Msafiri Safarini – M. K. Ghassani
- Wosia wa Baba – A.M. Amanzy

## 5. HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI.


- Historia ya Tanzania na Maadili, Shule za Sekondari, Kitabu cha Mwanafunzi, Kidato cha Tano – TIE
- Msingi wa Umahiri katika Historia ya Tanzania na Maadili, Kidato cha Tano – Makini Publishers.

## 6. ACADEMIC COMMUNICATION.

- Academic Communication, A guide for Advanced Level – Alex A.Mkunda
- Academic Communication, For Advanced Secondary Schools Students Book, Form Five – TIE

**MWONEKANO WA SARE YA MWANAFUNZI**






**MSHONO WA SURUALI**